**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI DESEMBA, 2021**

## 1.0 Utangulizi

Taarifa hii ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020) ni ya kipindi cha Julai – Desemba, 2021. Ilani hii imetekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwashirikisha Wananchi, Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wadau wengine chini ya usimamizi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi mbalimbali.

Maeneo yaliyotekelezwa na ambayo yanatolewa taarifa ni Kupambana na umaskini na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (Ibara ya 26): Maendeleo ya Wanawake na Vijana (Ibara ya 32); Vyama vya Ushirika (Ibara ya 34); Kilimo (Ibara ya 37) Ufugaji (Ibara ya 40); Uvuvi (Ibara ya 43): Viwanda (Ibara ya 46); Barabara (Ibara ya 55); Viwanja vya ndege (Ibara ya 59); Nishati ya Umeme (Ibara ya 63); Utalii (Ibara ya 67); Misitu (Ibara ya 69); Ardhi (Ibara ya 74); Maendeleo ya Elimu (Ibara ya 80); Huduma za Afya (Ibara ya 83); Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Mlipuko ikiwemo Corona; (Ibara ya 84); Lishe (Ibara ya 86); Ustawi wa Jamii, Ustawi wa Wazee, Wanawake na Watoto (Ibara ya 91); Huduma za Maji (Ibara ya 100); Ulinzi na Usalama na Masuala ya Vitambulisho vya Taifa kupitia NIDA (Ibara ya 105); Mapambano dhidi ya Rushwa na Ufisadi (Ibara ya 116); Ukusanyaji wa Mapato (Ibara ya 122); Utatuzi wa kero na malalamiko ya wananchi (Ibara ya 122); Ujenzi wa nyumba za Viongozi na Ofisi za Umma; Maendeleo ya Watumishi Ibara ya 130); Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Ilani, Namna Mkoa ulivyoshughulikia changamoto zilizojitokeza na Hitimisho.

Utekelezaji wa Ilani hii ulianza mwezi Julai, 2021 ambapo hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 takribani Shilingi bilioni **81** zimetumika.

Baada ya maelezo hayo, naomba nitoe Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha Julai-Desemba, 2021 kisekta kama ifuatavyo:-

## 2.0 Kupambana na umaskini na uwezeshaji wananchi kiuchumi (Ibara ya 26)

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika eneo la uwezeshaji wananchi kiuchumi katika kipindi cha Julai – Desemba, 2021 ni pamoja na kupambana na umaskini na:-

(i) Jumla ya Wajasiriamali **5,374** wamepatiwa elimu ya ujasiriamali katika Mkoa wa Iringa. Elimu hiyo ilitolewa na Wataalam wa Halmashauri, Taasisi zisizo za Serikali na Wataalamu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA). Aidha, wajasiriamali **2,900** wameweza kukuza uzalishaji na mitaji yao.

(ii) Jumla ya vibanda **250** vya biashara kwa ajili ya wafanyabiashara ndogo ndogo vimejengwa katika eneo la Mshindo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa. Ujenzi wa vibanda hivyo hadi sasa umegharimu Shilingi milioni **83.3**. Aidha, mradi huo ulianza kutekelezwa mwezi Oktoba, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2022.

(iii) Jumla ya Vijana **3,044** Wanawake **1,891** na watu wenye ulemavu **57** wamepatiwa mafunzo na stadi za ujasiriamali na usimamizi wa shughuli za kiuchumi.

(iv) Kufanyika kwa Kongamano la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Mkoani Iringa tarehe 22/11/2021. Kongamano hilo lilihudhuriwa na Wanawake **1,339**. Pamoja na mambo mengine, Kongamano hilo lilitumika kutoa elimu ya ujasiriamali, utunzaji wa familia na tuzo zilitolewa kwa Wanawake Wajasiriamali waliofanya vizuri.

(v) Kaya **25,632** za Mkoa wa Iringa zimeendelea kunufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) kwa mchanganuo ufuatao:- Halmashauri ya Manispaa ya Iringa Kaya 2,442, Halmashauri ya Mji Mafinga kaya 1,050, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo Kaya 9,788, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi Kaya 5307 na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Kaya 7,045.

Malipo kwa ajili ya kunusuru Kaya hizi yamefanyika ambapo jumla ya Shilingi milioni 911.4 zimetolewa kwa wanufaika wa Mpango kama ifuatavyo:- Halmashauri ya Manispaa Iringa Shilingi milioni 47.1, Halmashauri ya Mji Mafinga Shilingi milioni 40.3, Halmashauri ya Wilaya Kilolo Shilingi milioni 342.7, Halmashauri ya Wilaya Mufindi Shilingi milioni 205.9 na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Shilingi milioni 275.2.

**3.0 Maendeleo ya Wanawake na Vijana (Ibara ya 32)**

Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kwenye eneo la Maendeleo ya Wanawake na Vijana ni pamoja na:-

*(i)* Mikopo iliyotolewa kwa Vikundi vya Vijana ni Shilingi milioni **526.6** ambazo zilikopeshwa kwa Vikundi vya Vijana **49.** Mikopo hiyo iliyotolewa ni sawa na asilimia **114** ya lengo la kutoa mikopo ya Shilingi milioni **462.**

*(ii)* Mikopo iliyotolewa kwa Vikundi vya Wanawake ni Shilingi milioni **540.2** ambazo zilikopeshwa kwa Vikundi vya Wanawake **60.** Mikopo hiyo iliyotolewa ni sawa na asilimia **117** ya lengo la kutoa mikopo ya Shilingi milioni **462.8**

*(iii)* Mikopo iliyotolewa kwa Vikundi vya Watu wenye Ulemavu ni Shilingi milioni **73.8** ambazo zilikopeshwa kwa Vikundi vya Watu Wenye Ulemavu **22.** Mikopo hiyo iliyotolewa ni sawa na asilimia **20.4** ya lengo la kutoa mikopo ya Shilingi milioni **360.1**

(iv) Hivyo, jumla ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ni Shilingi bilioni **1.143** ambayo ni sawa na asilimia **71.1** ya fedha za mapato ya ndani zinazopelekwa kwenye Miradi ya Maendeleo (40%) ya mapato halisi ya ndani ya Halmashauri (own source proper) yaliyokusanywa katika kipindi hicho ambayo ni Shilingi bilioni **1.5.** Mikopo mingine inatarajiwa kuanza kutolewa mwezi Januari, 2022.

Jedwali kuonesha mchanganuo wa mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

| Halmashauri | Wanawake | Vijana | Watu Wenye Ulemavu | Jumla | Idadi Ya Vikundi | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Wanawake | Vijana | Watu Wenye Ulemavu | |
| Mufindi DC | 141,580,000 | 165,000,000 | 20,000,000 | 326,580,000 | 7 | 7 | 5 | 19 |
| Iringa Dc | 128,600,000 | 128,600,000 | 14,800,000 | 272,000,000 | 21 | 24 | 8 | 53 |
| Iringa MC | 57,000,000 | 26,000,000 | 9,000,000 | 92,000,000 | 11 | 7 | 5 | 23 |
| Kilolo DC | 94,000,000 | 105,000,000 | 5,000,000 | 204,000,000 | 9 | 5 | 1 | 15 |
| Mafinga TC | 119,028,625 | 102,028,663 | 25,000,000 | 249,169,140 | 12 | 6 | 3 | 21 |
| JUMLA KUU | **540,208,625** | **526,628,663** | **73,800,000** | **1,143,749,140** | **60** | **49** | **22** | **131** |

(v) Mwenendo wa urejeshaji wa fedha zilizokopeshwa kwenye vikundi husika kwa kipindi cha Julai-Desemba, 2021 ilikuwa inavyooneshwa kwenye jedwali Na.1

| Kiasi Kilichotolewa | Idadi ya Vikundi | Kiasi rejeshwa | Kiasi bado kurejeshwa |
|---|---|---|---|
| 1,068,028,626 | Wanawake 322<br>Vijana 142<br>Watu wenye ulemavu 38<br>**Jumla 502** | 396,274,500 | 671,754,126 |

Kati ya Shilingi milioni **396.3** zilizorejeshwa, Shilingi milioni **108.8** zilirejeshwa na Vikundi vya Wanawake, shilingi milioni **65.8** zilirejeshwa na Vikundi vya Vijana na Shilingi milioni **4.5** zilirejeshwa na Vikundi vya Watu Wenye Ulemavu. Aidha, ufuatiliaji wa urejeshaji wa kiasi kilichobaki unaendelea.

## 4.0 Vyama vya Ushirika (Ibara ya 33)

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Ushirika katika kipindi Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na:-

(i) Idadi ya Vyama vya Ushirika vilivyofufuliwa ni vinne (**4)** sawa na asilimia **50** ya lengo la kufufua Vyama nane (**8)**. Vyama vilivyofufuliwa ni pamoja na **Maduma AMCOS LTD** kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi**, Muungano Mtitu LTD na Mshikamano Ikuka LTD** vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya Kilolo **na Kihanga AMCOS LTD** kilichopo Halmashauri ya Wilaya Iringa**.**

(ii) Chama cha Msingi kimoja (**1)** kilianzishwa sawa na asilimia **10** ya lengo la kuanzisha vyama **10**. Chama kilichoanzishwa ni **Kilolo Tea Glowers Agricultural Marketing Cooperative Society (AMCOS**).

(iii) Mtaji wa Vyama vya Ushirika uliongezeka kutoka Shilingi bilioni **15.90** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Shilingi bilioni **15.96** mwezi Desemba, 2021. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia **0.38**. ya makadirio ya kuongeza mtaji wa Vyama Vya Ushirika kufikia Shilingi bilioni **16.**

(iv) Hadi kufikia mwezi Desemba 2021 jumla ya shilingi 13,483,424,000 zilikuwa zimetolewa na vyama 75 vya ushirika kama mikopo kwenda kwa wanachama wake

**5.0 Kilimo (Ibara ya 37)**

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Kilimo kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na: -

(i) Mkoa umeendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea ambapo kwa msimu wa Mwaka 2021 jumla ya tani **41,692.2** za mbolea ziliuzwa kwa wananchi. Mbolea zilizouzwa ni kwa ajili ya kupandia na kukuzia.

(ii) Uzalishaji wa mazao yote ya chakula kwa msimu wa 2020/2021 ulikuwa ni tani milioni **1.173** sawa na asilimia **89.4** ya lengo la kuzalisha tani milioni **1.313** ya mazao ya chakula. Mazao yaliyozalishwa ni pamoja na mahindi tani **784,524**, mpunga tani **75,995** na mazao mengineyo yakiwepo ngano, mtama, ndizi, mihogo, viazi vitamu, viazi mviringo, maharage, kunde, njegere, njugumawe na ulezi tani **313,031.**

(iii) Uzalishaji wa mazao ya Biashara kwa msimu wa 2020/2021 ulikuwa ni tani **51,300** sawa na asilimia **71.5** ya lengo la kuzalisha tani. **71,779**.

(iv) Ununuzi wa mahindi kupitia Wakala wa Serikali ilikuwa ni tani **2357.576**, ununuzi wa mahindi hayo ulifanyika kwenye vituo vya **Igomaa, Ilula, Ifunda** na **Kihorogota.** Aidha, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (Iringa) ilinunua mahindi tani milioni **1.5** kutoka kwa wakulima.

(v) Uhamasishaji kwa wananchi ili waweze kulima mazao ya kimkakati ambayo ni ufuta, alizeti, pareto, korosho na parachichi uliendelea kufanyika kwa kushirikiana na wadau. Aidha, uzalishaji wa mazao hayo kwa Mwaka 2021 ulikuwa kama ifuatavyo;

- Ufuta tani **376** kati ya lengo la kuzalisha tani **247** sawa na asilimia **152.**
- Alizeti tani **34,315** kati ya lengo la kuzalisha tani **52,573** sawa na asilimia **65.**
- Pareto tani **54** kati ya lengo la kuzalisha tani **47** sawa na asilimia **114.8.**
- Korosho tani **2** kati ya lengo la kuzalisha tani **16** sawa na asilimia **12.5**.
- Parachichi tani **994** kati ya lengo la kuzalisha tani **911** sawa na asilimia **109.**

Aidha, Bodi ya Korosho imetoa mbegu za korosho kilo **1,210** kwa ajili ya wakulima wa Halmashauri za Wilaya ya Iringa (Kilo 600) na Kilolo (Kilo 610). Lengo la kutoa mbegu hizo ni kuhamasisha kilimo cha zao la Korosho,

kuongeza uzalishaji na tija. Mbegu hizo zitapandwa kwenye msimu wa 2021/2022.

(vi) Mkoa uliratibu zoezi la upimaji wa udongo lililofanyika Mwaka 2021 ambapo vijiji 100 kati ya Vijiji 360 vya Mkoa wa Iringa vilipimwa udongo. Matokeo ya utafiti huo yaliwasilishwa kwenye Halmashauri zote tarehe 8/10/2021. Manufaa ya upimaji wa udongo kwa wananchi ni pamoja na:-

- Kufahamu hali/afya ya udongo.
- Kufahamu aina ya mbolea itakayotumika kulingana na aina ya mazao wanayoyalima.
- Kuongeza uzalishaji na tija.

(vii) Ukarabati wa Skimu za Mgambalenga, Msosa na Ruaha mbuyuni ulifanyika kwa kurejesha Mto Lukosi katika mkondo wake wa awali baada ya uharibifu uliotokana na mvua. Ukarabati huo uligharimu Shilingi milioni **87.9** ambazo zilitolewa na Serikali kupitia Tume ya Umwagiliaji.

(viii) Ukarabati wa Skimu za Magozi na Mlenge ulifanyika kwa kurejesha Mto Ruaha Mdogo katika mkondo wake wa awali. Ukarabati huo uligharimu Shilingi milioni **64.7** ambazo zilitolewa na Serikali kupitia Tume ya Umwagiliaji.

## 6.0 Ufugaji (Ibara ya 40)

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Ufugaji kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na:-

(i) Idadi ya Ng'ombe imeongezeka kutoka Ng'ombe **346,027** waliokuwepo Mwezi Juni, 2021 hadi kufikia ng'ombe **348 846** mwezi Desemba, 2021.

(ii) Idadi ya Mbuzi imeongezeka kutoka mbuzi **180,332** waliokuwepo Mwezi Juni 2021 hadi kufikia mbuzi **183,180** mwezi Desemba, 2021.

(iii) Idadi ya kondoo imeongezeka kutoka Kondoo **68,950** waliokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Kondoo **69,894** mwezi Desemba, 2021.

(iv) Majosho manne (4) ya Magana, Iyayi, Ikuka na Mtandika yaliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo yamekarabatiwa kwa gharama ya shilingi milioni 28,2. Majosho mawili **2** yanaendelea kukarabatiwa. Majosho yanayokarabatiwa ni Josho la Kitasengwa lililopo Kata ya Makungu na Josho la Ifwagi lililopo Kata ya Ifwagi (Majosho yote hayo yapo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi). Aidha, ukarabati huo utatumia jumla ya Shilingi milioni **4.6.**

(v) Majosho mapya mawili **2** yanaendelea kujengwa ambayo ni Josho la Idetelo lililopo Kata ya Mbalamaziwa na Josho la Kibada lililopo kata ya Kibada. Majosho yote hayo yapo Halmashauri ya Wilaya Mufindi. Aidha, jumla ya Shilingi milioni **15** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa majosho hayo.

(vi) Ujenzi wa Mnada mpya wa Mifugo wa Idunda Kata ya Idunda Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi unaendelea kwa gharama ya Shilingi milion**i 21**.

(vii) Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni **57.3** mwezi Juni 2021 hadi kufikia lita milioni **58.5** mwezi Desemba, 2021.

(viii) Uzalishaji wa mitamba bora ya maziwa na nyama umeongezeka kutoka mitamba **6,660** uliokuwa umefikia mwezi Juni, 2021 hadi kufikia mitamba **9,836** mwezi Desemba, 2021.

(ix) Mkoa umetambua na kusajiri ng'ombe, mbuzi na kondoo kwenye Mfumo wa Utambuzi Usajiri na Ufuatiliaji wa Mifugo kwa njia ya kuvalisha hereni za kielektroniki ambapo ng'ombe **7,338,** kondoo **112** na mbuzi **1,131** walisajiriwa katika kipindi hicho.

(x) Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa ya Ngelewala iliyopo Manispaa ya Iringa ulifikia asilimia **90** ya utekelezaji hadi mwezi Desemba, 2021 kutoka asilimia 50 iliyokuwa imefikiwa Mwezi Juni, 2021. Aidha, mradi huo unatarajiwa kukamilika Mwaka wa fedha 2021/2022.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha miundombinu inayoendelea kujengwa katika Machinjio ya Kisasa ya Ngelewala iliyopo Halmashauri ya Manispaa Iringa.



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa Jengo la Maabara katika Machinjio ya Kisasa ya Ngelewala iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa Jengo la Utawala katika Machinjio ya Kisasa ya Ngelewala iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa Mabwawa ya maji machafu katika Machinjio ya Kisasa ya Ngelewala iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa*

# ZIZI LA KUHIFADHIA WANYAMA WANAOTAKIWA KUCHINJWA



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa zizi la kuhifadhia Ng'ombe wanaotarajia kuchinjwa katika machinjio ya Kisasa ya Ngelewala iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa*

**7.0 Uvuvi (Ibara ya 43)**

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Uvuvi katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na: -

(i) Idadi ya Mabwawa yaliyochimbwa imeongezeka kutoka Mabwawa **2,008** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Mabwawa **2,152** mwezi Desemba, 2021.

.Ifuatayo ni moja ya picha ya mabwawa ambayo yameanzishwa



*Picha inayoonesha mradi wa Bwawa la Samaki wa Shule ya Msingi ya Igomaa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi*

(ii) Idadi ya vikundi vya Wavuvi vilivyoundwa ni **2** kati ya lengo la kuunda vikundi **4.** Vikundi vilivyoundwa vina jumla ya Wavuvi **37** na vimeundwa katika Halmashauri za Wilaya za Mufindi na Iringa,

(iii) Kiasi cha Samaki kilichovuliwa kimeongezeka kutoka tani **513.20** zilizovuliwa mwezi Juni 2021 hadi kufikia tani **845.63** zilizovuliwa mwezi Desemba, 2021. Aidha, mapato ya Serikali yaliyokusanywa kutokana na na shughuli za uvuvi kwa kipindi husika ni Shilingi milioni **36.5.**

**8.0 Sekta ya Viwanda (Ibara ya 46)**

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Viwanda katika kipindi husika ni pamoja na:-

(i) Viwanda vikubwa viwili **(2)** vinaendelea kujengwa katika Mkoa wa Iringa.Viwanda hivyo ni LUSH CHANZO kilichopo Halmashauri ya Mji Mafinga ambacho kitajihusisha na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya misitu, na kingine ni Kiwanda cha Kuzalisha Chakula cha Mifugo kinachojengwa na SHAFA Agro Company katika eneo la Kidamali katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Kiwanda cha LUSH CHANZO kikikamilika na kuanza uzalishaji kitaajiri watu kati ya 450 hadi 700 na kile cha SHAFA kitaajiri takribani watu 200.

(ii) Idadi ya Viwanda Vidogo imeongezeka kutoka Viwanda **443** vilivyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Viwanda vidogo **460** mwezi Desemba, 2021 ikiwa ni ongezeko la viwanda vidogo **17** ambavyo vimezalisha ajira kwa watu **148.**

(iii) Idadi ya Viwanda Vidogo imeongezeka kutoka Viwanda **1,351** vilivyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Viwanda Vidogo **1,375** mwezi Desemba 2021 ikiwa ni ongezeko la viwanda vidogo **24** ambavyo vimezalisha ajira kwa watu **224.**

**9.0 Barabara (Ibara ya 55)**

### 9.1 Matengenezo ya Barabara kupitia Wakala ya Barabara Nchini (TANROADS)

Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 Serikali kupitia Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) Mkoa wa Iringa ilitoa jumla ya Shilingi bilioni **4.8** ambazo zimetumika kutengeneza barabara zenye urefu wa km **33.1** na madaraja manne (4). Aidha, miradi iliyotekelezwa na TANROADS katika kipindi husika ni pamoja na:-

(i) Ukarabati wa Barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa km 1.4 ambao umegharimu Shilingi bilioni **1.2** Ukarabati huo umefanyika kwenye barabara zifuatazo:-

- Ugwachanya (Tosamaganga Junction) – Hospitali ya Tosamaganga **(Km 1.4)** ujenzi wa tuta la barabara tabaka la chini na ujenzi wa makalvati umekamilika na maandalizi ya tabaka la lami yanaendelea.
- Barabara ya Iringa bypass (Kihesa Kilolo-Tumaini- Igumbilo) ambapo ujenzi wa madaraja manne (4) kati ya sita (6) umekamilika na kazi inaendelea.

(ii) Matengenezo ya kawaida na ya vipindi maalum katika barabara za lami zenye urefu wa km **7.4** ambayo yamegharimu kiasi cha Shilingi bilioni **1.7** Barabara zilizokarabatiwa ni pamoja na:-

- Iringa – Mtera (eneo la Igingilanyi) (km 3.5**),** kazi ambayo imefanyika ni ujenzi wa tuta la barabara tabaka la chini ambao umekamilika na maandalizi ya tabaka la lami yanaendelea.
- Ipogolo – Idete (Ndiwili – Kilambo) **(km 3.9)** ujenzi wa tuta la barabara tabaka la chini unaendelea.

(iii) Matengenezo ya kawaida na ya vipindi maalum katika barabara za changarawe zenye urefu wa km 24 ambayo yamegharimu jumla ya Shilingi milioni **486.** Malipo kwa wakandarasi hayajafanyika kwasababu kazi inaendelea.

(iv) Ujenzi wa barabara ya Ipogolo – Idete umeongezeka kutoka **km 15.94** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia **km 16.14** mwezi Desemba, 2021. Ujenzi huo umegharimu Shilingi milioni **188.1.**

(v) Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mafinga – Mgololo imefikia asilimia **95** (kazi ipo hatua za mwisho za kuandaa makabrasha ya zabuni na imegharimu Shilingi milioni **116.7.**

Zifuatazo ni baadhi ya picha za *miradi iliyotekelezwa na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) katika kipindi cha Julai- Desemba, 2021.*



*Picha inayoonesha upanuzi wa Barabara eneo la Idete katika Halmashauri ya Wilaya Kilolo*



*Picha inayoonesha upanuzi wa Barabara eneo la Idete katika Halmashauri ya Wilaya Kilolo*



*Picha inayoonesha kazi ya kuweka Tabaka la chini (CRR) ikiwa inaendelea eneo la Igingilanyi katika Barabara ya Iringa- Dodoma*



*Picha inayoonesha Ujenzi wa daraja katika barabara ya mchepuo ya Kihesa Kilolo-Tumaini-Igumbilo eneo la Chuo kikuu cha Iringa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.*

## 9.2. Ujenzi wa Barabara Kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA)

Mafanikio yaliyopatikana kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA**)** kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na: -

(i) Ujenzi wa barabara za lami umeongezeka kutoka **Km 116.20** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia **Km 133.88** mwezi Desemba, 2021. Ujenzi huo umegharimu Shilingi bilioni **12.8**. Ongezeko hilo la ujenzi wa barabara ni sawa na asilimia **15.21** ya makadirio ya kuongeza km **53.25** za barabara za lami. Barabara za lami zilizojengwa ni pamoja na Kidabaga – Bomalang'ombe, Sawala – Mkonge – Iyegeya, Makondeko – Ndolezi na Mwamkoa – Mbagala.

(ii) Ujenzi wa barabara za Changarawe umeongezeka kutoka Km **1,894.268** zilizokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Km **1,993.066** mwezi Desemba, 2021 ambazo zimegharimu Shilingi bilioni **1.02**. Barabara za changarawe zilizojengwa ni **15** kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho "A".**

(iii) Ujenzi wa barabara za udongo umeongezeka kutoka Km **3,343.15** zilizokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Km **3,458.825** mwezi Desemba, 2021 ambazo zimegharimu Shilingi milioni **853.4.** Barabara za udongo zilizojengwa ni **22** kama zinavyoonekana kwenye **Kiambatisho "B".**

(iv) Ujenzi wa madaraja umeongezeka kutoka madaraja **382** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia madaraja **399** mwezi Desemba, 2021 ambayo yamegharimu jumla ya Shilingi milioni **962.1.** Madaraja makubwa yaliyojengwa ni pamoja na;-

- Daraja la Ifwagi kwenye barabara ya Itona - Ifwagi
- Daraja la wami kwenye barabara ya Vikula – Kilosamufindi
- Ilula – Ilambo
- Mtandika – Nyanzwa
- Makungu – Mlafu na Itimbo – Kitelewasi
- Mtwivila Darajani.

(iv) TARURA imepokea Shilingi bilioni **3.5** ikiwa ni fedha za majimbo (bilioni **2.1**) na tozo za miamala ya simu (bilioni **1.4**) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya barabara ambapo barabara **31** zinatekelezwa kupitia fedha za majimbo na barabara **25** zinatekelezwa kupitia fedha za tozo. Barabara hizo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho "C".**

(v) TARURA imepokea kiasi cha Shilingi bilioni **1.3** kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara ya Ifunda-Bandabichi-Itengulinyi iliyopo katika Halmasghauri ya Wilaya ya Iringa. Utekelezaji wa barabara hiyo umefikia asilimia 80.

Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) inaendelea kutekeleza Miradi mikubwa ya Barabara kwa kutumia fedha za ndani na za Wafadhili kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa barabara ya Sawala –Mkonge –Iyegeya (km 30.3) chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya umefikia Km **12.3** kutoka km **6** zilizokuwa zimejengwa kufikia mwezi Juni, 2021. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2021 "**first seal"** imekamilika kwenye "km 1.9 na kuchanganya kifusi na saruji ili kuimalisha tabaka la barabara (stabilization) kumekamilika kwenye eneo la km 16.1.

- Ujenzi wa Barabara ya Kidabaga-Bomalang"ombe (km 18.3) chini ya ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya umefikia km **18.3** kutoka Km **12** zilizokuwa zimejengwa kufikia mwezi Juni, 2021.

- Ujenzi wa daraja la Tosamaganga umefikia asilimia **75** kutoka asilimia **20** zilizokuwa zimefikiwa mwezi Juni, 2021.

- Ujenzi wa barabara ya Makondeko – Ndolezi (km 0.8) umefikia km **0.75** kutoka km **0.6** zilizokuwa zimejengwa kufikia mwezi Juni, 2021.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha miradi ya barabara inayotekelezwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) katika kipindi cha Julai- Desemba 2021;-



*Picha inayoonesha uchanganyaji wa Chokaa kwenye barabara ya kidabaga – Bomalang'ombe iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo*



*Picha inayoonesha ujenzi wa daraja box kalvati la midomo minne katika barabara ya Ilula – Ilambo (Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo)*



*Picha inayoonesha ujenzi wa daraja katika barabara ya Ifunda – Bandabichi katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea katika Barabara ya Mtwivila - Darajani – Ikonongo (Manispaa ya Iringa)*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea katika Barabara ya Donbosco-Mawelewele-Zizi (Manispaa ya Iringa)*

**10.0 Viwanja vya Ndege (Ibara ya 59)**

Kwa upande wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:-

i. Upanuzi wa barabara ya kurukia na kutua ndege umefikia asilimia **35** ikilinganisha na asilimia **15** iliyokuwa imefikiwa mwezi Juni, 2021.

ii. Hatua ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali ambayo ni pamoja na Jengo la Muda la Abiria, Jengo la Zimamoto na "power house umefikia asilimia **26** ukilinganisha na asilimia **0** mwezi Juni, 2021.

iii. Hadi mwezi Desemba, 2021 gharama zilizotumika kwenye ujenzi wa barabara ya kuruka ndege na miundombinu mingine ni Shilingi bilioni **10.9**.

iv. Ujenzi wa barabara ya kuruka ndege na miundombinu mingine kulingana na mkataba unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2024.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha hatua iliyofikiwa kwa baadhi ya miradi inayotekelezwa katika eneo la Uwanja wa Ndege wa Iringa



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa njia ya kurukia na kutua ndege kwenye Uwanja wa Ndege wa Iringa*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa Jengo la muda la abiria (Terminal Building) katika uwanja wa Ndege wa Iringa..*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa Jengo la ‘‘power house’’ katika uwanja wa Ndege wa Iringa.*

## 11.0 Nishati ya Umeme (Ibara ya 63)

Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 Serikali ilitoa jumla ya Shilingi bilioni **3.8** kwa ajili ya usambazaji wa umeme kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Iringa.

Kiasi hicho kilitumika katika kusambaza umeme kwenye jumla ya maeneo (59). Maeneo yaliyopatiwa umeme yalihusisha mashamba manne (**4)** pampu za maji mbili (**2)**, Mitaa 10 Vitongoji 30, Shule za Msingi tatu (3), Sekondari tano (5), Makanisa matatu (3) na Misikiti miwili (2).

Aidha, zoezi la usambazaji umeme vijijini nalo liliendelea ambapo hadi kufikia Desemba, 2021 jumla ya vijiji **324** vilikuwa vimepatiwa umeme kati ya vijiji **360** vilivyopo Mkoani Iringa. Vijiji vilivyobaki ni **36** ambavyo vipo katika mchanganuo ufuatao:-

- Wilaya ya Iringa Vijiji sita (6)
- Wilaya ya Kilolo Vijiji ishirini na moja (21)
- Wilaya ya Mufindi Vijiji tisa (9)

Aidha, Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) limejiwekea mkakati wa kuhakikisha kuwa Vijiji vyote vinapatiwa umeme kwa kukamilisha kazi ya usambazaji umeme katika vijiji vyote vilivyobakia katika mradi wa REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (REA III Round II 36/37) ifikapo Desemba, 2022.

## 12.0 Utalii (Ibara ya 67)

Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 Mkoa umeendelea kuboresha mazingira ya kutembelewa na Watalii yatakayowezesha Watalii wa ndani na nje kutembelea Vivutio vilivyopo Mkoani Iringa. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi husika kwenye Sekta ya Utalii ni pamoja na:-

(i) Uhamasishaji kwa wananchi na wageni kutembelea Vivutio vilivyopo Mkoani Iringa ulifanyika kwa kushirikiana na wadau. Aidha, jumla ya watalii **9,073** walitembelea vivutio vilivyopo Mkoani Iringa. Kati ya Watalii hao, Watalii wa ndani walikuwa **4,762** na watalii wa nje wataalam ("expatriet") walikuwa **1,284** na watali wa kawaida "Non Residents" walikuwa **3,027**.

(ii) Mkoa umeratibu maadhimisho ya Wiki ya Utalii Duniani kwa kutoa mafunzo ya Utalii kwa Shule za Msingi **52** na Sekondari **27** lengo likiwa ni kujenga uelewa mpana kwa wanafunzi kuhusiana na Utalii. Aidha, Mkoa umetoa hamasa kwa wananchi kutembelea vivutio kupitia vyombo vya habari.

(iii) Aidha, GN inayoruhusu matumizi ya eneo la Kihesa Kilolo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Kiutalii imetoka tarehe 7/1/2022. GN hiyo inaruhusu kutekelezwa kwa Mpango wa matumizi ya eneo hilo. Matumizi ya eneo hilo yanatarajiwa kuanza rasmi Mwaka huu wa fedha wa 2021/2022.

(iv) Serikali kupitia Program ya REGROW inaendelea kutekeleza kazi ya upembuzi yakinifu wa Barabara zitakazojengwa kwenye hifadhi ya Ruaha ili kuyafikia maeneo yenye vivutio yasiyofikika.

Aidha, kupitia programu ya REGROW inayohusisha matengenezo ya Barabara katika hifadhi za ukanda wa Kusini ambazo ni Ruaha, Udzungwa na Mikumi, upembuzi yakinifu wa barabara zilizopo katika hifadhi hizo unaendelea kufanyika ambapo, utagharimu Shilingi bilioni **2.3.** Program imetoa mitambo **8** yenye thamani ya Shilingi bilioni **12** ambayo inatumika katika kufanya matengenezo ya Barabara katika Hifadhi ya Ruaha.

## 13.0 Sekta ya Misitu (Ibara ya 69)

Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 Mkoa umeendelea kusimamia shughuli zinazohusu Sekta ya Misitu. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho kwenye Sekta ya Misitu ni pamoja na:

(i) Mkoa kwa kushirikiana na wadau, umehamasisha upandaji na utunzaji wa miti. Matokeo ya uhamasishaji huo yanaonesha kuwa, kati ya miti milioni **34.3** ilipandwa katika kipindi cha Januari-Juni, 2021, miti milioni **31.7** ilitunzwa na kupona ikiwa ni sawa na asilimia **92.6** ya miti iliyopandwa.

(ii) Kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha Sekta ya Misitu kuzalisha ajira kwa wananchi. Katika kutekeleza jukumu hili Mkoa uliratibu Kongamano la Uwekezaji katika Sekta ya Misitu na Maonesho ya Bidhaa za Misitu Katika Vwanja vya Wambi Mafinga tarehe 13 hadi 15/11/2021. Lengo la Kongamano na maonesho hayo, lilikuwa ni kutangaza fursa zilizopo kwenye Sekta ya Misitu, kuhamasisha uwekezaji utakaozalisha ajira na kuitangaza Sekta ya Misitu nje na ndani ya Mkoa wa Iringa.

Jumla ya wajasiriamali **90** walishiriki katika maonesho hayo na Wananchi wapatao **1,200** walishiriki katika Kongamano hilo.

(iii) Uwezo kwa wadau wa Utalii, Misitu, wanyamapori, Mazingira, Nyuki umeimarishwa kupitia vikao mbalimbali lengo likiwa ni kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki ili kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Mkoa. Tarehe 20-21/12/2021 wadau **50** wa misitu walijengewa uwezo wa utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za misitu ikiwa ni pamoja na ufugaji wa nyuki. Vilevile tarehe 23-24/9/2021 wadau **60** wa utalii walijengewa uwezo wa kuendeleza Sekta ya Utalii katika kuhamasisha watalii wa ndani na nje kutembelea vivutio vilivyopo katika Mkoa wa Iringa.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha Washiriki wa Kongamano la Misitu la Mkoa wa Iringa lililofanyika tarehe 13-15/10/2021 na mafunzo kwa wadau wa nyuki.



*Picha inayoonesha baadhi ya washiriki wa Kongamano la Misitu la Mkoa wa Iringa lilofanyika tarehe 13-15/11/2021 Katika Viwanja vya Wambi vilivyopo Halmashauri ya Mji Mafinga*




*Picha inayoonesha baadhi ya Viongozi walioshiriki katika Kongamano la Misitu la Mkoa wa Iringa lilofanyika tarehe 13-15/11/2021 katika viwanja vya Wambi vilivyopo Halmashauri ya Mji Mafinga*

**14.0 Ardhi (Ibara ya 74)**

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Ardhi katika kipindi cha Julai – Desemba, 2021 ni pamoja na:-

(i) Kutolewa kwa jumla ya hati **12,156** hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 kupitia Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa iliyoanzishwa mwaka 2020. Ofisi hiyo imerahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma ya masuala ya ardhi kwa wananchi.

(ii) Jumla ya viwanja **5,914** na mashamba **42** yamepimwa katika kipindi hicho.

(iii) Jumla ya Hatimiliki za Kisheria **1,574** na Hati za Kimila **10,582** zimetolewa

(iv) Urasimishaji wa makazi **703** umefanyika katika Halmashauri mbili (2), ambazo ni Halmashauri ya Mji Mafinga makazi **664** na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa makazi **39**.

(v) Kiasi cha Shilingi bilioni **1.09** kimekusanywa kutokana na kodi za ardhi kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021.

(vi) Migogoro mikubwa miwili (2) ya Ardhi imesuluhishwa kati ya mitatu **(3)** iliyoripotiwa. Migogoro iliyosuluhishwa ni pamoja na:-

  (i) Mgogoro kati ya **Jeshi la Magereza Mlolo** dhidi ya ndugu **Modestus Kalinga**

  (ii) Mgogoro kati ya **Jumuiya ya Waislam Chuo Kikuu cha Tumaini** (Iringa) dhidi ya familia za **Erick Mgeni na George Fuime**

**15.0 Maendeleo ya Elimu (Ibara 80)**

Mafanikio yaliyopatikana kwenye Sekta ya Elimu kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021 ni pamoja na:-

**15.1 Elimu ya Awali**

(i) Upatikanaji wa vifaa vya kufundisha na kujifunzia umeongezeka kutoka asilimia **65.2** mwezi Juni, 2021 hadi asilimia **65.7** mwezi Desemba, 2021.

**15.2 Elimu ya Msingi**

(i) Mkoa ulipokea kiasi cha Shilingi bilioni **1.8** zilizotolewa na Serikali chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19. Kati ya fedha hizo zilizotolewa Shilingi bilioni **1.64** zilikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **82** katika Shule Shikizi za Msingi na Shilingi milioni **160** kwa ajili ya Ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa Elimu Maalum katika shule za Msingi Amani iliyopo Halmashauri ya Mji Mafinga na Shule ya Msingi Kisilasi iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

| NA. | HALMASHAURI | FEDHA ILIYOTOLEWA | FEDHA ILIYOTUMIKA | IDADI YA MADARASA/MABWENI YALIYOJENGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOBAKI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | IRINGA MC | - | - | 0 | - |
| 2. | IRINGA DC | 560,000,000.00 | 560,000,000.00 | 28 | - |
| 3. | KILOLO DC | 240,000,000.00 | 240,000,000.00 | 12 | - |
| 4. | MUFINDI DC | 920,000,000.00 | 840,000,000.00 | 43 | - |
| | MAFINGA TC | 80,000,000.00 | 73,952,927.52 | 1 | 6,047,072.48 |
| | **JUMLA** | **1,800,000,000.00** | **1,713,952,927.52** | **84** | **6,047,072.48** |

Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya madarasa na mabweni yaliyojengwa kwenye Shule Shikizi kupitia Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.



*Picha inayoonesha vyumba viwili (2) vya madarasa na Ofisi vilivyojengwa katika Shule Shikizi ya Idodi Mtambula katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi*.



*Picha ya madarasa mawili (2) yaliyojengwa katika Kituo Shikizi cha Itotoma Kata ya Mninga Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.*



*Picha inayoonesha jengo lenye vyumba viwili (2) vya madarasa katika Kituo Shikizi Umoja Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*



*Picha inayoonesha jengo lenye vyumba viwili (2) vya madarasa katika Kituo Shikizi Lutitili-Kibena, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.*



*Picha inayoonesha jengo la bweni la wanafunzi wa Elimu Maalumu linaloendelea kujengwa katika Shule ya Msingi Amani, Halmashauri ya Mji Mafinga,*



*Picha inayoonesha jengo la bweni la wanafunzi wa Elimu Maalumu linaloendelea kujengwa katika Shule ya Msingi Kisalasi, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi*

(ii) Idadi ya Madarasa ya Elimu Msingi imeongezeka kutoka madarasa **4,313** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi madarasa **4501** mwezi Desemba, 2021.

(iii) Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka matundu **8,277** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi matundu **8,360** mwezi Desemba, 2021.

(iv) Idadi ya madawati katika Shule za Msingi imeongezeka kutoka madawati **86,343** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Madawati **93,837** mwezi Desemba, 2021.

(v) Idadi ya Shule za Msingi zimeongezeka kutoka shule **525** zilizokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Shule **537** mwezi Desemba, 2021. Shule zilizoongezeka ni **Kisada, Malendi, Igominyi, Ifiga, Kidilu, Igeme, Kilumbwa, Mwangaza, Umoja na Ilawa** zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na Shule za **Ukwega na Itunundu B** zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

(vi) Hali ya ufaulu kwa matokeo ya Darasa la saba (PSLE)-2021 yaliyotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania yanaonesha kuwa Mkoa wa Iringa umeshika nafasi ya Pili kati ya Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Aidha, Mkoa ulikuwa na Watahiniwa **28,016** na waliofaulu ni **25,498** sawa na asilimia **91.01**.

### 15.3. Elimu ya Sekondari

(i) Mkoa ulipokea Shilingi bilioni **4.9** zilizotolewa na Serikali chini ya Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba **245** vya madarasa katika Shule za Sekondari.

| NA. | HALMASHAURI | FEDHA ILIYOTOLEWA | FEDHA ILIYOTUMIKA | IDADI YA MADARASA/MABWENI YALIYOJENGWA | KIASI CHA FEDHA KILICHOBAKI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | IRINGA MC | 660,000,000.00 | 660,000,000.00 | 33 | - |
| 2. | IRINGA DC | 1,320,000,000.00 | 1,320,000,000.00 | 66 | - |
| 3. | KILOLO DC | 1,460,000,000.00 | 1,460,000,000.00 | 73 | - |
| 4. | MUFINDI DC | 1,140,000,000.00 | 1,140,000,000.00 | 57 | - |
| | MAFINGA TC | 320,000,000.00 | 320,000,000.00 | 16 | - |
| | JUMLA | **4,900,000,000.00** | **4,900,000,000.00** | **245** | - |

Zifuatazo ni baadhi ya picha za vyumba vya madarasa vilivyojengwa kupitia Mradi wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 katika Mkoa wa Iringa: -



*Picha inayoonesha jengo lenye vyumba vitano (5) vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Lukosi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo*



*Picha inayoonesha jengo lenye Vyumba viwili (2) vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Tagamenda katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa*



*Picha inayoonesha jengo lenye madarasa mawili (2) na Ofisi ya Walimu katika Shule ya Sekondari ya Kinyanambo katika Halmashauri ya Mji Mafinga.*




*Picha inayoonesha jengo lenye darasa katika Shule ya Sekondari ya Furahia iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa*.

(ii) Mkoa ulipokea Shilingi milioni **325** zilizotolewa na Serikali kutokana na Tozo ya Miamala ya Simu. Fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **26** katika Shule za Sekondari. Ukamilishaji wa maboma hayo upo katika hatua mbalimbali.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha miradi iliyotekelezwa kupitia fedha zilizotokana na Tozo za Miamala ya Simu:-



*Picha ikionesha ukamilishaji wa maboma katika Shule ya Sekondari Nyololo iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.*



*Picha ikionesha ukamilishaji wa maboma katika Shule ya Sekondari Kiheka iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*



*Picha inayoonesha kazi ya Umaliziaji wa ujenzi wa Madarasa mawili (2) Shule ya Sekondari ya Kalenga katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.*



*Picha inayoonesha kazi ya Umaliziaji wa ujenzi wa Madarasa Shule ya Sekondari ya Changarawe iliyopo Halmashauri ya Mji Mafinga.*

(iii) Idadi ya vyumba vya madarasa imeongezeka kutoka vyumba vya madarasa **1,632** vilivyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia madarasa **1,956** mwezi Desemba, 2021.

(iv) Idadi ya Shule za Sekondari imeongezeka kutoka Shule **185** zilizokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Shule **189** mwezi Desemba, 2021. Shule zilizoongezeka ni Saint **GIOVANO**, **EDUCA**, **MEDALA** na **KENASY** Shule zote hizo zipo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

(v) Idadi ya nyumba za walimu wa Sekondari zilizojengwa imeongezeka kutoka nyumba **605** zilizokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia nyumba **609** mwezi Desemba, 2021.

(vi) Idadi ya Maabara imeongezeka kutoka maabara **227** zilizokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia maabara **247** mwezi Desemba, 2021. Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha Maabara zilizojengwa katika kipindi husika:-



*Picha inayoonesha eneo la ndani la Maabara iliyojengwa katika Shule ya Sekondari ya Mivinjeni Idunda iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.*



*Picha inayoonesha jengo la Maabara katika Shule ya Sekondari ya Itengule iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.*

(vii) Idadi ya madawati katika Shule za Sekondari imeongezeka kutoka madawati **64,664** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia madawati **69,834** mwezi Desemba, 2021.

(viii) Idadi ya matundu ya vyoo imeongezeka kutoka matundu **2,677** yaliyokuwepo mwezi Juni, 2021 hadi kufikia matundu **2,777** yaliyojengwa kufikia mwezi Desemba, 2021.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha baadhi ya vyoo vilivyojengwa katika kipindi husika:-



*Picha inayoonesha Matundu 10 ya vyoo yaliyojengwa katika Shule ya Sekondari ya Kiheka, iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*



*Picha inayoonesha Jengo la Choo katika Shule ya Sekondari ya Bumilayinga, iliyopo Halmashauri ya Mji Mafinga.*

(ix) Ufaulu wa mtihani wa Kidato cha Sita Kimkoa umepanda kutoka asilimia **99.43** mwaka **2020** hadi kufikia asilimia **99.72** mwaka **2021.**

### 15.4. Elimu Bila Malipo

Jumla ya Shilingi bilioni **4.1** zimepokelewa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Elimu Bila Malipo katika kipindi cha Julai-Desemba, 2021. Kati ya kiasi hicho kilichopokelewa Shilingi **1.2** zimetumika kwenye Shule za Msingi na Shilingi **2.9** zimetumika kwenye Shule za Sekondari.

### 15.5. Miradi inayotekelezwa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa

Katika kipindi cha Julai-Desemba, 2021 Serikali ilitoa kiasi cha Shilingi bilioni **3.3** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwenye Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Miradi inayotekelezwa kupitia fedha hizo ni pamoja na:-

**(i) Upanuzi wa Juu wa Maabara ya Viumbe Hai**

Mradi huo ulianza kutekelezwa mwezi Juni, 2021 na unakusudiwa kutumia Shilingi milioni **864.2** na unatarajia kukamilika mwezi Februari, 2022. Aidha, hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 mradi huo ulikuwa umefikia asilimia 75 na ulikuwa umetumia Shilingi milioni **262.2.** Jengo hilo likikamilika litapunguza uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Zifuatazo ni picha zinazoonesha hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Mradi wa upanuzi Maabara ya Viumbehai:-



*Picha inayoonesha muonekano wa nje wa jengo la Maabara ya Viumbehai linaloendelea kujengwa katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa*



*Picha inayoonesha muonekano wa ndani wa jengo la Maabara ya Viumbehai linaloendelea kujengwa katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa*

**(ii) Ukarabati wa majengo na miundombinu ya Chuo**

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kinaendelea kutekeleza shughuli ya ukarabati mkubwa wa majengo na miundombinu ya Chuo. Katika Awamu ya Kwanza ya ukarabati jumla ya majengo 13 yaliwekwa kwenye mpango wa ukarabati. Majengo hayo ni:- mabweni ya wanafunzi (majengo matano), Ukumbi Mkuu wa Mikutano (majengo matatu), Jengo la Ofisi za Utawala, Jengo la Udahili, jengo la Maabara ya Kemia namba tatu na majengo ya Maabara za Kompyuta/Sayansi (majengo mawili).

Ukarabati huo ulitegemea kugharimu Shilingi milioni **300**. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2021 kazi ya ukarabati wa majengo yote ulikuwa umefikia asilimia **85** na ulikuwa umetumia kiasi cha Shilingi milioni **243**.

Ukarabati huo ukikamilika utasaidia kuyarudisha majengo yaliyochakaa katika hali nzuri na hivyo kuongeza ufanisi katika ufundishaji na utumiaji rasilimaliwatu (wahadhiri) na kupunguza uhaba wa miundombinu ya kufundishia, kujifunzia na malazi.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha baadhi ya majengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa baada ya kukarabatiwa



*Picha inayoonesha jengo la Maabara ya Kemia lililopo katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa baada ya kukarabatiwa.*



*Picha inayoonesha Jengo la Maabara za Sayansi/Kompyuta katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa*

**(iii) Mradi wa ujenzi wa barabara ndani za ndani ya Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Mkwawa**

Ujenzi wa barabara za ndani ya Chuo zenye urefu wa Kilomita **3.8** unaendelea ikiwa ni utekelezaji wa agizo la aliyekuwa Rais wa Serikali ya awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayani Dkt. John Pombe Magufuli alipotembelea Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa tarehe 2/5/2018.

Mradi huo unasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na unatekelezwa na Mkandarasi Mtwivila Traders&Construction Co.Ltd kwa grarama ya Shilingi bilioni **3.08**.

Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021 mradi huo ulikuwa umefikia asilimia **94** ya utekelezaji. Hivyo, mradi huo umekamilika kwa kiasi kikubwa (substantial completion) na barabara zimeanza kutumika.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zinazoonesha mradi wa ujenzi wa barabara za ndani katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa:-



*Picha inayoonesha sehemu ya mzunguko wa barabara iliyojengwa katika Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa*



*Picha inayoonesha sehemu ya Barabara Na. 1 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa*

## 16.0 Huduma za Afya (Ibara ya 83)

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Afya kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na: -

i. Mkoa wa Iringa ulipokea kiasi cha Shilingi bilioni **1.75** zilizotolewa na Serikali kutokana na Tozo za Miamala ya Simu ili kujenga Vituo vya Afya saba (7) katika Halmashauri tano za Mkoa wa Iringa. Vituo hivyo ni Mkimbizi kilichopo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Malengamakali na Kiwele vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Ifingo kilichopo Halmashauri ya Mji Mafinga, Sadani na Kibengu vilivyopo Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Nyalumbu kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo. Ujenzi wa Vituo vyote saba umeshaanza na upo katika hatua mbalimbali.

   Zifuatazo ni baadhi ya picha za ujenzi unaoendelea kwenye Vituo vya Afya husika:-



*Picha inayoonesha jengo la wagonjwa wa nje likikamilishwa katika Kituo cha Afya cha Mkimbizi katika Manispaa ya Iringa.*



*Picha inaonesha Jengo la huduma za wagonjwa wa nje likiwa linakamilika, katika Kituo cha Afya Ifingo, Halmashauri ya Mji wa Mafinga.*



*Picha inayoonesha hatua iliyofikiwa katika Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje Kituo cha Afya Kibengu, Halmashauri ya wilaya Mufindi.*



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa jengo la Maabara katika Kituo cha Afya Nyalumbu, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*

ii. Mkoa wa Iringa ulipokea Shilingi milioni **800** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya Zahanati katika Halmashauri zote. Tayari maboma matatu (3) katika Halmashauri ya Wilaya Kilolo (Mbawi, Masege na Lugalo) yamekamilika. Aidha, maboma matatu (3) katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi (Igombavanu, Kiyowela na Ihanu) yamekamilika. Kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa Iringa vituo viwili vya Mtalagala na Itamba vimekamilika. Vilevile Jengo la Wagonjwa wa Nje katika Kituo cha Afya cha Ifingo Halmashauri ya Mji Mafinga limekamilika.

Zifuatazo ni baadhi ya picha za ujenzi unaoendelea kwenye Zahanati husika



*Picha inayoonesha Jengo la zahanati ya Lugalo baada ya kukamilika, lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*



*Picha inayoonesha Jengo la zahanati ya Igombavanu, likiwa limekamilika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.*



*Picha ikionesha jengo la OPD la Zahanati ya Mtalagala likiwa limekamilika kwa asilimia 95, Manispaa ya Iringa.*

*iii.* Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilitoa Shilingi milioni **600** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Huduma za Dharura (EMD) katika Hospitali za Halmashauri ya Mji Mafinga na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Taratibu za kuwapata wajenzi/wazabuni wa kujenga miundombinu hiyo zinaendelea

*iv.* Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilitoa kiasi cha Shilingi milioni **250** kwa ajili ya ujenzi wa Chumba cha Huduma ya Wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo. Taratibu za kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea.
Aidha, Shilingi milioni **150** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa chumba cha wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na tayari taratibu za manunuzi zimeanza. Vilevile, jumla ya Shilingi milioni **770** zimetengwa kupitia Wizara ya Afya kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vitakavyotumika katika chumba hicho.

*v.* Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi milioni **852** kwa ajili ya ununuzi wa Mashine za Mionzi katika Hospitali za Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Halmashauri za Wilaya za Iringa na Kilolo,
Vilevile Shilingi milioni **420** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kisasa ya Mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa. Taratibu za ununuzi wa mashine hizo zinaendelea kupitia Wizara ya Afya.

Aidha, Serikali katika mwaka 2021/2022 imetenga jumla ya Shilingi bilioni **2.18** kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya CT- Scan itakayofungwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa. Mashine hiyo ikifungwa itasaidia sana kupunguza adha ya wananchi kufuata huduma katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Benjamini Mkapa iliyoko Dodoma.

*vi.* Katika mwaka wa fedha wa 2021/22, Serikali imetoa jumla ya Shilingi milioni **360**, kupitia Mradi wa UVIKO – 19, kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Watumishi wa Afya kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Iringa (milioni **90**), Kituo cha afya cha Ruaha – Mbuyuni (milioni **90**) na Hospitali ya Wilaya ya Mufindi (milioni **90**)na hospitali ya Rufaa (milioni **90**). Halmashauri zote zinaendelea na taratibu za kuwapata wajenzi wa nyumba hizo.

*vii.* Serikali katika mwaka wa fedha 2021/22, imetoa fedha Shilingi bilioni **3.1** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kilolo Shilingi milioni **800,** Hospitali ya Wilaya ya Iringa Shilingi milioni **800**, Hospitali ya Wilaya ya Mufindi milioni **800** na Hospitali ya Manispaa ya Iringa – FRELIMO Shilingi milioni **700.** Taratibu za ujenzi zitaanza baada ya kupokelewa kwa maelekezo stahiki kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI

.

viii. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitoa kiasi cha Shilingi bilioni **1.8** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya vitano (5) vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya mbili za Kilolo na Iringa. Kituo cha afya Migoli kimepokea Shilingi milioni **400**, Ismani Shilingi milioni **400**, Ilula Shilingi milioni **400**, Ruaha – Mbuyuni Shilingi milioni **300** na Kibena Shilingi milioni **300**. Ujenzi katika vituo vya Afya vitatu (Ismani, Migoli na Ilula) uko katika hatua ya umaliziaji.

Vituo vya afya vya Ruaha Mbuyuni na Kibena vinaendelea na taratibu za awali za utangazaji wa zabuni.

Zifuatazo ni baadhi ya picha zikionesha hali ya utekelezaji wa miradi iliyopokea Shilingi bilioni **1.8**:-



*Picha inayoonesha ujenzi wa jengo la Wodi ya wazazi yenye chumba cha Upasuaji katika kituo cha Afya cha Ilula, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*



*Picha inayoonesha ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa wa Nje (OPD) katika Kituo cha Afya Ilula, Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo*.

ix. Kwa mwaka 2021/2022 Ujenzi wa jengo la Huduma za Dharura (EMD) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa umekamilika, ambapo jumla ya Shilingi milioni **621** zimetumika. Serikali pia imetenga Shilingi milioni **691.5** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

x. Katika kipindi cha mwaka 2021/22, Ujenzi wa Jengo la Maabara ya Vifaa Tiba Saidizi/ Viungo Bandia (Orthopaedic Laboratory) uliofadhiliwa na Mdau ASAS Company Ltd kwa kushirikiana na ASVET (Vicenza) uliogharimu jumla ya Shilingi Milioni **300**, ulikamilika na kukabidhiwa kwa Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa tayari kwa usimikaji mitambo na kuanza kutumika.

Ifuatayo ni Picha inayoonesha jengo jipya la Maabara ya Viungo Bandia lililojengwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa



*Picha inayoonesha jengo jipya la Maabara ya Vifaa Tiba Saidizi/ Viungo Bandia katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa.*

xi. Upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya umeongezeka kutoka asilimia **78.3** mwezi Juni 2021 hadi kufikia asilimia **88** mwezi Desemba, 2021.

xii. Vituo vya Afya vipya viwili (2) vimeongezeka katika kipindi husika ambavyo ni Kituo cha Afya cha Ruaha Mbuyuni kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo (Kituo cha Serikali) na Kituo cha Afya cha binafsi cha DRL kilichopo Halmashauri ya Mji Mafinga.

xiii. Idadi ya Wagonjwa waliopata huduma za Kibobezi na Kibingwa imeongezeka kutoka wananchi **47,807** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia wananchi **50,397** mwezi Desemba, 2021. Aidha, huduma za kibingwa na Kibobezi zimekuwa zikitolewa kwa utaratibu wa wagonjwa kupewa rufaa kuja Hospitali ya Rufaa, kuwaleta madaktari bingwa toka Hospitali za Muhimbili na Benjamini Mkapa kuja Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na pia kutembelea Hospitali za Halmashauri.

xiv. Kiwango cha utoaji wa huduma za Afya ya Mama na Mtoto katika vituo vyote kimefikia asilimia **91** mwezi Desemba, 2021.

xv. Kiwango cha upatikanaji wa huduma tembezi na mkoba kwa mama na mtoto kimeongezeka kutoka asilimia **93** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia asimilia **95** mwezi Desemba, 2021.

xvi. Kiwango cha upatikanaji wa damu salama kimeongezeka kutoka asilimia 78 mwezi Juni, 2021 hadi kufikia asilimia 90 mwezi Desemba, 2021. (Chupa 293 kwa mwezi).

xvii. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021, kiwango cha Kaya zilizokuwa na Choo Bora (Improved Latrine) kilikuwa ni asilimia **83.9** kati ya Kaya zote za Mkoa wa Iringa.

xviii. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2021, kiwango cha Kaya zilizokuwa na vifaa vya msingi vya unawaji mikono (uwepo wa maji yanayotiririka na sabuni) kilikuwa ni asilimia **72**, ya kaya zote za Mkoa wa Iringa.

xix. Idadi ya Vijiji vilivyothibitishwa kuwa na ubora wa usafi (Open Defaecation – Free Certified Villages) iliongezeka toka Vijiji **31** mnamo mwaka 2020 hadi kufikia Vijiji **189** Desemba, 2021,

**17.0 Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Mlipuko ikiwemo UVIKO - 19 (Ibara ya 84)**

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta hii ni pamoja na:

i. Wataalam **550** wamepatiwa mafunzo ya kutibu magonjwa ya mlipuko hadi kufikia mwezi Disemba, 2021.

ii. Idadi ya walengwa waliopata na kukamilisha chanjo ya UVIKO – 19 katika kipindi cha Julai – Disemba 2021 ni **27,763** kati ya walengwa **706,396**, sawa na asilimia **3.9**. Aidha, Mkoa ulipokea jumla ya chanjo **88,017** ikiwa ni pamoja na chanjo ya Jensen Jensen (24,485), Sinopharm (51,832) na Pfizer (11,700). Aidha, jumla ya chanjo **52,838** zilitolewa kwa wananchi.

iii. Idadi ya vifaa/vitendea kazi vya kutibu magonjwa ya mlipuko vilivyotolewa imeongezeka kutoka vifaa/vitendea kazi **15,783** mwezi Juni,2021 hadi kufikia vifaa/vitendea kazi **26,820** mwezi Disemba, 2021.

iv. Idadi ya Vituo vya Kisasa vya kuwatenga wahisiwa wa COVID- 19 imeongezeka kutoka vituo saba (**7)** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia vituo **13** mwezi Desemba, 2021. Baadhi ya vituo vilivyoongezeka ni pamoja na Kituo cha Afya cha **Wenda,** Kituo cha Afya cha **Ngome**, Kituo cha Afya cha **Nyololo**, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na Kituo cha Afya cha **Ihongole** kilichopo Halmashauri ya Mji Mafinga.

**18.0 Lishe (Ibara ya 86)**

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya lishe katika kipindi cha Julai-Desemba, 2021 ni pamoja na :-

(i) Ukondefu kwa Watoto chini ya miaka mitano (5) umeshuka hadi kufikia asilimia 3 mwezi Desemba, 2021.

(ii) Idadi ya wataalam wa afya waliojengewa uwezo wa kutoa huduma za lishe imeongezeka kutoka wataalam **718** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia wataalam **899** mwezi Disemba, 2021.

(iii) Kiasi cha Fedha zilizotengwa na Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa Afua za Lishe hadi kufikia Desemba, 2021 ni Shilingi milioni **112.9** kati ya fedha hizo zilizotolewa ni Shilingi milioni **62.5** sawa na asilimia **55**. Utengaji wa fedha na utoaji kwenye afua za Lishe unaendelea kutekelezwa kwenye Halmashauri.

(iv) Shughuli muhimu za lishe zilizofanyika katika kipindi cha Julai-Desemba, 2021 ni pamoja na:-

- Kufanya ziara za Usimamizi Shirikishi na Elekezi kwenye vituo vya huduma za lishe
- Kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba ya Lishe.
- Maadhimisho ya siku ya Afya na Lishe na kutoa elimu na unasihi juu ya Lishe na afya hufanyika kila baada ya miezi sita.

(v) Mashirika, Taasisi na Asasi zilizoshiriki kikamilifu katika kutoa elimu na uhamasishaji wa lishe ni pamoja na:-

- USAID Save The Children
- CALL AFRICA
- WORLD VISION
- CUAM/CEFA
- ALLAMANO
- PAPA YOHANE
- THE GLOBAL VOLUNTEER
- TAHEA
- ASAS Co. Ltd

## 19.0 Ustawi wa Jamii, Wazee, Wanawake na Watoto (Ibara ya 91)

Mafanikio yaliyopatikana kwenye Sekta hii ni pamoja na:-

(i) Idadi ya Wazee wanaopatiwa huduma za Matibabu Bila Malipo imeongezeka kutoka wazee **33,976** mwezi Juni 2021 hadi kufikia Wazee **38,315** mwezi Desemba, 2021.

(ii) Kiwango cha kuimarika kwa Huduma za Matibabu Bila Malipo kwa Wazee kimeongezeka kutoka asilimia **73** Mwezi Juni, 2021 hadi kufikia asilimia **81** mwezi Desemba, 2021.

(iii) Idadi ya Mabaraza ya Wazee yaliyoimarishwa imeongezeka kutoka Mabaraza **299** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Mabaraza **311** mwezi Disemba, 2021.

(iv) Idadi ya Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zilizoundwa imeongezeka kutoka Kamati **206** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Kamati **286** mwezi Desemba, 2021.

(v) Idadi ya Watoto waliofanyiwa vitendo vya kikatili imepungua kidogo kutoka watoto **175** mwezi Juni 2021 hadi kufikia watoto **154** mwezi Desemba, 2021. Jitihada zaidi za kupambana na ukatili dhidi ya watoto zinaendelea kuchukuliwa kwenye Halmashauri zote.

(vi) Idadi ya Mabaraza ya Watoto yaliyoimarishwa imeongezeka kutoka Mabaraza **221** mwezi Juni, 2021 hadi Mabaraza **236** mwezi Disemba, 2021

(vii) Idadi ya Wanawake waliofanyiwa vitendo vya kikatili imepungua kutoka Wanawake **821** mwezi Juni, 2021 hadi kufikia Wanawake **111** mwezi Desemba, 2021. Hata hivyo, jitihada zaidi za kupambana na ukatili dhidi ya wanawake zinaendelea kuchukuliwa ili kutokomeza vitendo vya ukatili kwa wanawake katika Halmashauri zote.

(viii) Hali ya ukatili kwa wanaume kwa Mkoa wa Iringa imefikia matukio **36** mnamo Disemba 2021. Hata hivyo, jitihada zaidi za kupambana na ukatili dhidi ya wanaume zinaendelea kuchukuliwa ili kutokomeza vitendo vya ukatili kwa wanaume katika Halmashauri.

## 20.0 HUDUMA ZA MAJI (Ibara ya 100)

Kwa upande wa Sekta ya Maji katika kipindi cha Julai-Desemba, 2021 Sekta ya Maji Mkoa wa Iringa imetekeleza miradi kama ifuatavyo:-

**Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini**

(i) Imeweza kukamilisha miradi 12 kwenye Vijiji 11 ambavyo vipo kwenye mchanganuo ufuatao:- Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo miradi 6 ambayo ni Mgowelo, Kipaduka, Kiwalamo, Magana, Kitowo na Ihimbo. Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi miradi iliyokamilishwa ni 6 ambayo ni Kasanga, Udumuka, Nyololo njia panda, Uhambila, Ikweha na Ikimilinzowo.

(ii) Miradi 12 inaendelea na utekelezaji katika Halmashauri kwa mchanganuo ufuatao:- Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo miradi mitano (5), Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi miradi mitatu (3) na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa miradi minne (4).Utekelezaji wa miradi hiyo umetumia kiasi cha Shilingi bilioni **3.7**.

(iii) Kupitia kwa wadau ambao ni "Water for Africa" wamewezesha uchimbaji wa visima 18 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi (visima 14) na Halmashauri ya Mji Mafinga (visima 4). Visima hivyo vimechimbwa katika Shule za msingi, Sekondari na Zahanati.

(iv) Serikali imetoa fedha kiasi cha Shilingi bilioni **3.76** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ikiwemo mradi wa Ruaha Mbuyuni ambao kwa sasa umetekelezwa kwa asilmia 85 na kugharimu Shilingi Bilioni **1.4**, Ukarabati wa mradi wa maji Malangali ambao upo katika hatua ya usanifu, Malizanga 5%, Mgowelo 100%, ukarabati wa mradi wa Tungamalenga( hatua ya usanifu) , Kibena, Ihemi,

Ujenzi mradi wa Nyamlenge Lot 1( Ndiwili na Kilambo) 85% Mradi wa Nyabula Mlanda, Makotopola mbwelili, Makuka, Lumuli -Itengulinyi, Ujenzi wa mradi wa maji Kimala, Ifua, Uhambingeto, Masalali Wilaya ya Kilolo Ipo katika hatua za ununuzi wa wakandarasi ambayo ipo kwenye bajeti ya mwaka 2021-2022.

(v) Miradi **10** ya maji na usafi wa mazingira inaendelea kutekelezwa kwenye Vijiji **22** chini ya programu ya **NWF, PforR na PbR**. Miradi hiyo hadi kukamilika kwake inatarajia kugharimu kiasi cha Shilingi bilioni **5.03.** Miradi hiyo inatekelezwa kwenye vijiji vya Image, Mtandika, Ruaha Mbuyuni, Msosa, Vitono, Mawambala, Malangali, Mtwango, Magunga, Ndiwili, Kilambo, Idodi, Ufyambe, Mwilavila, Itengule, Sadani Kihata, Tambalang'ombe, Isikinyi, Kingege, Ihowanza, Idumulavanu, Ipilimo na Ikangawani. Miradi hiyo inatarajia kukamilika mwaka wa fedha 2021/2022 na inakusudia kuwahudumia wananchi **49,304**.

Kutokana na jitihada hizo, mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

- Hali ya upatikanaji wa maji safi na salama katika Mkoa imefikia asilimia **79.6** Aidha, jumla ya watu **1,193,313** wanapata huduma ya maji safi na salama ambapo wakazi wa Vijijini wanaopata huduma ya maji safi imefikia asilimia **73.61.**
- Jumuiya za watumiaji wa maji zimefikia **81** na idadi ya vituo vya kuchotea maji Vijijini vimefikia **5,743** ambapo kati ya vituo hivyo vinavyofanya kazi ni vituo **4,780** na vina uwezo wa kuhudumia wananchi **669,452** waishio Vijijini.

**Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini (IRUWASA)**

Huduma ya usambazaji maji safi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Iringa, Mji wa Kilolo na Mji wa Ilula, inatolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA). Huduma ya majisafi kwa Manispaa ya Iringa imewafikia asilimia 97 ya wakazi wa Manispaa ya Iringa, wakati huduma hii imewafikia asilimia 67 ya wakazi wa Kilolo Mjini na asilimia 84 ya wakazi wa Ilula Mjini.

Katika kuhakikisha huduma ya maji inaboreka katika Manispaa ya Iringa, Miji ya Kilolo na Ilula, IRUWASA inatekeleza miradi ifuatayo;

i. **Mradi wa usambazaji maji maeneo ya pembezoni mwa Mji**

(a) **Mradi unaofadhiliwa na IFF – OBA kwa kushirikiana na IRUWASA**

- Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya Shilingi bilioni **2.5** ambazo ni mkopo kutoka TIB (Tanzania Investment Bank) kiasi cha Shilingi Bilioni 1.6 kupitia mpango unaoratibiwa na Wizara ya Maji wa *Ifrastructure Investiment Financing – Output Based Aid* (*IFF – OBA*) huku IRUWASA ikichangia Shilingi milioni 900. Asilimia hamsini ya Mkopo pamoja na mchango wa IRUWASA, italipwa na KfW chini ya program hiyo pale IRUWASA itakapokamilisha malengo ya mradi huo.

(b) **Mradi wa uboreshaji huduma ya Maji Isimani – Kilolo**

Mradi huo ni miongoni mwa miradi ya kupeleka huduma ya maji kwenye maeneo ya pembezoni ambao unataraji kuwahudumia zaidi ya wananchi 58,000 kwa sasa na zaidi ya 80,000 ifikapo 2038 katika jumla ya vijiji 29 (kilolo 5 na Isimani 24).

Mradi huo unagharimu Shilingi bilioni **9.2** (kiasi kilichotolewa ni Shilingi bilioni **4.2**) na mradi umefikia asilimia **55** ya utekelezaji ambapo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022.

- **Mamlaka ya Maji n Usafi wa Mazingira Mjini Mafinga (MAUWASA)**

Kwa upande wa Mamlaka ya majisafi na usafi wa Mazingira Mafinga (MAUWASA), imepanga kutekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika mji wa Mafinga awamu ya pili utakaohusisha upanuzi wa mtandao wa maji eneo lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya uwekezaji (Makalala Investment Centre). Mradi huu utagharimu kiasi cha Shillingi milioni **120** fedha kutoka Serikali kuu kupitia Wizara ya Maji. Mradi huu uko kwenye hatua za mwisho za upatikanaji wa wazabuni. Vilevile Mamlaka imefanya ukarabati wa miundombinu ya maji eneo la Soko Kuu Mafinga, Mkombwe, Barabara ya wachaga, eneo la mashine ya mpunga, barabara ya eneo la Wambi na eneo la pipeline. Mradi huu wa ukarabati miundombinu umekamilika na umegharimu kiasi cha Shilingi milioni **15** ikiwa ni mapato ya ndani ya Mamlaka.

**Miradi chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19.**

Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imetenga fedha zaidi ya Shilingi bilioni **3.5** kwa ajili ya kutekeleza miradi mitano (5) katika Sekta ya Maji Mkoa wa Iringa chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19.

Miradi hiyo itatekelezwa kwenye Majimbo yote ya Uchaguzi ya Mkoa wa Iringa kama inavyooekana kwenye **kiambatisho E.**

Zifuatazo ni picha zinazoonesha baadhi ya Miradi ya Maji inayotekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA)



*Picha ya Tenki la Maji lililojengwa katika Mradi wa Maji wa Image katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.*



*Picha inayoonesha Kituo cha kuchotea Maji (DP) katika Mradi wa Maji wa Magunga uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.*

**21.0. Ulinzi na Usalama na Masuala ya Vitambulisho vya Taifa kupitia NIDA (Ibara ya 105)**

Katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Mkoa wa Iringa iliweka lengo la kuandikisha Wananchi **20,160,** ambapo Wananchi **3,445** walijitokeza na kuweza kuandikishwa sawa na asilimia **17.0** ya lengo lililowekwa.

Tangu zoezi la utoaji Vitambulisho lilipoanza mwaka 2017 jumla ya Wananchi **265,120** wa Mkoa wa Iringa wamepatiwa vitambulisho kati ya wananchi **506,606** walioandikishwa sawa na asilimia **52.3**

Ili kuongeza idadi ya wanaosajiliwa Ofisi ya NIDA Mkoa wa Iringa imeweka mikakati ya kutembelea shule za Sekondari na Vyuo ili kuandikisha wanafunzi waliofikisha umri wa miaka 18.

Kwa upande wa utoaji vitambulisho vya Taifa, Ofisi ya NIDA Mkoa imeendelea kugawa vitambulisho kwa kadri inavyopokea kutoka Makao Makuu, ambapo katika kipindi cha Julai - Desemba Ofisi ilipokea vitambulisho **101,383** ambavyo viligawiwa kwa wananchi husika kupitia Ofisi zao za Kata.

**22.0 Mapambano Dhidi ya Rushwa na Ufisadi (Ibara ya 116)**

Katika kipindi cha Julai – Desemba, 2021 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa imefanikiwa kutekeleza yafuatayo;

(i) Jumla ya Wananchi **13,543** wamepatiwa elimu ya mapambano ya rushwa kwa njia za mikutano ya Hadhara **45**, Semina **26**, Vipindi vya Redio **07**, Maonesho **02** na taarifa kwa umma (Press Release) **02.**

(ii) Jumla ya Vilabu vya Kupinga Rushwa **81** vimeanzishwa ambapo Vilabu **43** vimeanzishwa katika Shule za Msingi na vilabu **38** kwenye Shule za Sekondari.

(iii) Wananchi wameendelea kuelimishwa juu ya umuhimu wa kutoa taarifa na kuwafichua wote wanaojihusisha na rushwa. Kutokana na jitihada hizo jumla ya taarifa **70** zilipokelewa. Taarifa hizo zilizopokelewa ziliwezesha kufunguliwa kwa kesi **03** Mahakamani.

(iv) Idadi ya watu **04** walihukumiwa kifungo Gerezani kwa makosa ya rushwa. Aidha, jumla ya kesi **10** zinaendelea na usikilizwaji katika Mahakama.

**23.0 Ukusanyaji wa Mapato (Ibara 122)**

Katika kipindi cha Januari - Desemba, 2021 ukusanyaji wa Mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Nchini *(Tanzania Revenue Authotity - TRA)* Mkoa wa Iringa umefikia Shilingi bilioni **30.1** kati ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni **34.8.** Kiasi hicho kilichokusanywa ni sawa na asilimia **86 .7** ya lengo. Sababu za kutofikia lengo ni pamoja na:-

(i) Ucheleweshaji wa malipo ya VAT kwa baadhi ya walipa kodi wakubwa wanaojishugulisha na biashara ya mazao ya misitu kama vile nguzo za umeme. Jambo hilo linachangiwa na ucheleweshaji wa malipo kutoka kwa wateja wao ambao ni TANESCO na REA,

(ii) Baadhi ya wafanyabiashara wenye madeni kushindwa kulipa malipo yao kulingana na mikataba waliyokubaliana. Jitihada za kukusanya kodi hizo zinaendelea kufanyika.

Aidha, ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mkoa wa Iringa umefikia Shilingi bilioni **13.2** kati ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni **23.7.** Kiasi hicho kilichokusanywa ni sawa na **55.7%** ya lengo.

Halmashauri zimeendelea kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Baadhi ya Miradi iliyopewa fedha za mapato ya ndani ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 2

**JEDWALI NA.2 BAADHI YA MIRADI ILIYOTUMIA MAPATO YA NDANI YA HALMASHAURI**

| Na. | HALMASHAURI | JINA LA MRADI | FEDHA ILIYOTENGWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Halmashauri ya Wilaya Mufindi | Kituo cha Afya Ihowanza<br><br>Matengenezo stendi ya Nyololo | 300,000,000/=<br><br>29,000,000/= |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya Kilolo | Kituo cha Afya Ng'uruhe<br><br>Uendelezaji wa zao la Parachichi<br>Ukarabati wa majosho katika vijiji vitatu (3) | 100,000,000/=<br><br>47,770,000/=<br>28,200,000/= |
| 3 | Halmashauri ya Mji Mafinga | Kituo cha Afya Bumilayinga<br><br>Ununuzi wa maeneo ya uwekezaji<br>Ukamilishaji wa madarasa 6 ya Shule za Sekondari<br>Uendelezaji zao la parachichi | 165,000,000/=<br><br>120,000,000/=<br>85,500,000/=<br>17,600,000/= |
| 4 | Halmashauri ya Manispaa Iringa | Ujenzi wa Vibanda vya wafanyabiashara ndogondogo<br><br>Ukamilishaji wa jengo la Abiria stendi ya Igumbilo<br>Umaliziaji wa madarasa 11 | 62,000,000/=<br><br>56,000,000/=<br>40,400,000/= |
| 5 | Halmashauri ya Wilaya ya Iringa | Ununuzi wa gari la Halmashauri<br><br>Ujenzi wa nyumba za kupangisha<br>Ununuzi wa pikipiki 15 za watendaji wa Kata | 115,000,000/=<br><br>137,000,000/=<br>37,500,000/= |

## 24.0 Utatuzi wa Kero na Malalamiko ya Wananchi (Ibara ya 122)

Katika kipindi husika Mkoa uliendelea na utaratibu wa kusikiliza malalamiko na kero za wananchi ambapo kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021 jumla ya kero/malalamiko **275** yalipokelewa na kushughulikiwa kama ifuatavyo:-

(i) Ngazi ya Mkoa jumla ya kero/malalamiko **18** yalipokelewa, kero/malalamiko **14** yametatuliwa na kero/malalamiko 4 yanaendelea kushughulikiwa katika ngazi ya Mkoa.

(ii) Ofisi za Wakuu wa Wilaya zilipokea jumla ya kero/malalamiko **175**. Aidha, kero/malalamiko **117** yametatuliwa na kero/malalamiko **58** yanaendelea kushughulikiwa katika Ofisi hizo.

(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa zilipokea kero/malalamiko **82**. Kero/malalamiko **58** yametatuliwa na kero/malalamiko **24** yanaendelea kushughulikiwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**25.0 Ujenzi wa nyumba za Viongozi na Ofisi za Umma (Ibara ya 122)**
Katika kipindi cha Julai - Desemba 2021 miradi ya ujenzi wa nyumba za Viongozi na Ofisi za Umma imetekelezwa. Baadhi ya miradi hiyo iliyotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga umekamilika. Ujenzi huo hadi kukamilika kwake umegharimu kiasi cha Shilingi milioni **150.**

Ifuatayo ni picha inayoonesha nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga baada ya kukamilika.



*Picha inayoonesha nyumba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga baada ya kukamilika*

(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilipokea fedha za ujenzi wa jengo la Utawala kiasi cha Shilingi bilioni **1.** Fedha iliyotumika ni Shilingi milioni 839.6. Aidha, ujenzi wa awamu ya kwanza umefika asilimia 65.

Ifuatayo ni picha inayoonesha hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa jengo hilo



*Picha inayoonesha hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.*

(iii) Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipokea fedha za ujenzi wa jengo la Utawala kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Halmashauri hiyo kiasi cha Shilingi bilioni **1.** Aidha, ujenzi wa jengo hilo upo katika hatua ya kumwaga zege kwenye msingi.



*Picha inayoonesha ujenzi unaoendelea wa jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.*

(iv) Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ilipokea Shilingi milioni **95** kutoka kwa Mdau Salim Abri Asas kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Mstahiki Meya. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, ukarabati huo ulikuwa umekamilika kama inavyoonekana kwenye picha ifuatayo:-.



*Picha inayoonesha Jengo la Ofisi ya Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa baada ya kukamilika kwa ukarabati.*

**26.0 Maendeleo ya watumishi (Ibara ya 130)**

Baadhi ya mambo yaliyofanyika kuhusiana na watumishi katika kipindi cha Julai - Desemba, 2021 ni pamoja na;

(i) Jumla ya watumishi **234** wamelipwa malimbikizo ya mishahara yao yenye jumla ya Shilingi milioni 498.8**.**

(ii) Watumishi wapatao **176** waliopo Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa walipandishwa vyeo. Watumishi hawa ni sehemu ya Watumishi ambao hawakupandishwa Vyeo mwezi Juni 2021. Hadi sasa jumla ya watumishi **4,624** wamepandishwa vyeo kati ya watumishi **4,656** walipaswa kupandishwa vyeo sawa na asilimia **99**.

(iii) Watumishi wapya **194** wameajiriwa katika Sekta mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwemo Sekta za Afya, Elimu, Utawala Kilimo na ujenzi. Kati ya Watumishi hao walioajiriwa Halmashauri zetu zimeweza kuajiri Wahandisi **5**.

(iv) Halmashauri zilikuwa na mashauri ya kinidhamu **85**. Mashauri **81** yamehitimishwa na mashauri **4** yanaendelea kufanyiwa kazi kwenye Halmashauri.

**27.0 Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha Julai- Desemba 2021**

Katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kipindi cha Julai - Desemba 2021 zilijitokeza changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

(i) Kupanda kwa bei ya mbolea za viwandani hivyo, kuathiri uwezo wa wakulima kumudu gharama za mbolea hizo.

(ii) Kupanda kwa bei za vifaa vya viwandani hususan vifaa vinavyotumika kwenye ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

(iii) Baadhi ya Miradi inayotarajiwa kujengwa kwa kuwatumia Wakandarasi kama vile, ujenzi wa Vyumba vya Uangalizi kwa Wagonjwa Mahututi (ICU) kukosa Wakandarasi wanaohitajika (Daraja la Nne) kutokana na Wakandarasi hao kuomba kazi wa bei kubwa

(iv) Baadhi ya mafundi kukosa uaminifu na uwajibikaji hivyo, kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa kutekelezwa.

(v) Uchomaji wa misitu katika Halmashauri ya Mufindi,Kilolo na Mafinga hali ambayo inaleta hasara kwa wamiliki wa mashamba hayo na kupunguza kipato cha Halmashauri na kwa wamiliki wa mashamba.

## 28.0 Namna Mkoa ulivyoshughulikia changamoto zilizojitokeza

Katika kukabiliana na changamoto hizo Mkoa umefanya yafuatayo;

(i) Kuhamasisha wakulima kujiunga kwenye ushirika ili kuweza kuagiza mbolea kwa pamoja kwa bei yenye punguzo. Aidha, kuendelea kuhamasisha matumizi ya mbolea za samadi na mbolea za maji ambazo zina bei nafuu. Vilevile, wananchi wanahamasishwa kutumia mbolea ya Minjingu ambayo inauzwa bei nafuu.

(ii) Mkoa uliratibu utaratibu wa ununuzi wa pamoja wa vifaa vya ujenzi hususan vifaa vya utekelezaji wa Miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Kwa kiasi kikubwa utaratibu huo uliwezesha upatikanaji wa vifaa vya viwandani kwa bei nafuu.

(iii) Kurudia kutoa matangazo ili kuwapata Wazabuni wenye bei nafuu jambo ambalo linachelewesha utekelezaji wa Miradi.

(iv) Kuimarisha usimamizi wa Miradi ili kuhakikisha mafundi wanakuwepo kwenye maeneo ya miradi muda wote na miradi inatekelezwa kwa kasi na ubora uliokusudiwa.

(v) Katika kutatua changamoto ya baadhi ya Miradi kukosa Wakandarasi hususan katika ujenzi wa ICU, Serikali imetoa Mwongozo wa kutumia mfumo wa Force account kwa Halmashauri ambazo hazijapata Wakandarasi

(vi) Katika kutatua changamoto ya uchomaji mashamba misitu ya miti ya mbao, Mkoa umeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na kuepuka uanzishaji holela wa moto na udhibiti wake pindi unapotokea, pia Mkoa umepanga kukutana na Viongozi wa Mkoa wa Morogoro kwaajili ya kuweka mikakati ya pamoja juu ya udhibiti wa matukio ya moto kichaa.

## 29.0 Hitimisho

Uongozi wa Mkoa unatoa shukrani za dhati kwa Serikali Kuu, Taasisi za Serikali, Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Wananchi, Sekta Binafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mchango na ushirikiano mkubwa waliotupatia katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha Julai - Desemba 2021.

Aidha, Uongozi wa Mkoa unatoa shukrani za pekee kwa Uongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote kwa ushirikiano, ushauri, maelekezo na usimamizi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika kipindi cha Julai - Desemba

2021. Mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mzuri uliopo baina ya Chama cha Mapinduzi na Serikali. Tunawashukuru sana kwa uongozi wenu na ushirikiano wenu mzuri.

Naomba kuwasilisha.

Queen Cuthbert Sendiga
**MKUU WA MKOA**
**IRINGA**